

**Nafasi ya Misemo katika Jamii ya Wairaqw nchini
Tanzania**

Asha Shaaban
Chuo Kikuu Huria cha Tanzania

Gerephace Mwangosi
Chuo Kikuu Katoliki Ruaha
gerephacem@gmail.com

Ikisiri

Makala haya yamechunguza dhamira za misemo katika jamii ya Wairaqw nchini Tanzania kwa kudokeza namna mifumo ya maisha ya jamii inavyoakisiwa katika kazi za kifasihi kwa kurejelea utanze teule wa misemo ya jamii ya Wairaqw hapa nchini. Data za msingi zilikusanywa katika misemo ya jamii ya Wairaqw kwa mbinu za mahojiano na majadiliano. Lugha za Kiswahili na Kiiraqw zilitumika katika mahojiano, majadiliano na unukuzi wa data. Mbinu ya uteuzi lengwa ilitumika kupata watafitiwa waliosaidia kupata na kutafsiri data zilizokusanywa. Uchambuzi na mjadala wa data zilizowasilishwa umeongozwa na nadharia ya Usosholojia. Dhamira zilizochunguza hutumika kama maktaba mahsusini ya urejelezi wa masuala ya kijamii na kiungo thabiti cha kiasili kinachojenga mfumo wa kuifunza, kuiimarisha na kuiweka jamii pamoja katika misingi ya utamaduni na falsafa nzima ya maisha tangu kale mpaka sasa. Mwisho, misemo ni matendo ya msingi ya binadamu; na ni mojawapo ya vyombo thabiti vya kijadi vinavyopewa uwanja mpana katika kutekeleza, kuongoza na kutoa elimu kuhusu tabia na mienendo inayohitajika katika jamii.

Maneno Muhimu: Jamii ya Wairaqw, misemo, Tanzania

1.0 Utangulizi

Kijiografia, jamii ya Wairaqw inapatikana katika mikoa ya Manyara na Arusha (Karatu) iliyopo Kaskazini mwa Tanzania (Kamera, 1988). Kihistoria, Wairaqw walitokea Mesopotamia nchini Iraq katika Bara la Asia. Inasemekana walianza kuhama kati ya karne ya nne na sita baada ya kuzaliwa kwa Kristo. Wairaqw ni jamii ya Wakush, ambao walivuka bahari ya Shamu kwa mashua na kutua nchini Ethiopia (Pilot, 1999). Nchini Ethiopia waliishi kwa muda, lakini kutokana na vita vya mara kwa mara waliendelea kuhama kuelekea Kusini Magharibi kupitia bonde la ufa kando ya Ziwa Victoria hadi mpakani mwa Dodoma na Iringa wakitokea Iramba – Singida.

Vilevile, Wairaqw walielekea Kaskazini hadi Kondoa sehemu inayoitwa Guser Tuwalay. Waliishi hapo wakiwa wafugaji na wakulima wadogo. Baada ya kushindwa vita baina yao na Wabarbaik, Wairaqw walikimbilia karibu na mlima Hanang' na wengine walielekea Galapo (Tsea' Daa'w) (Thornton, 1980). Wairaqw waliwakuta Wagoroa ambao walielekea Mlima Dabil hadi Guse na Gangaru, ambapo walifanya maskani. Kiongozi wao anayeitwa *Haymu Now*, katika ukoo wa Haytipe, ndiye aliwaongoza hadi Nou na walifanya maskani yao katika maeneo ya Mamaisara. Inasemekana eneo lote la Mamaisara lilikuwa ziwa wakati ule. Hivyo, Wairaqw walifanya makazi katika maeneo ya milima. Baadaye Wairaqw waliendelea kutawanyika katika maeneo ya Muray, Kuta, Amoa, Kainam, Datlaa, Tsaa'yo katika Wilaya ya Mbulu.

Kiutawala, Wairaqw walikuwa na uongozi ulioanzia katika ngazi ya familia, ukoo hadi kufikia jamii nzima. *Kahamusmo* ndiye aliyekuwa kiongozi mkuu wa jamii ya Wairaqw. Kiongozi msaidizi alijulikana kama *Yaabusmo*. Kila mmoja alifanya kazi kwa nafasi yake ili kujimudu kifamilia na

kimaisha. Jamii hiyo hupenda kushirikiana katika shughuli zote za uzalishaji mali, uchumi na ujenzi wa jamii yao. Baadhi ya mila na desturi zao zinaelekeana na zile za Wayahudi, hasa katika matumizi ya kondoo katika masuala yanayohusu matambiko (Norbustad, 2002). Kondoo ni mnyama anayeheshimika sana katika jamii hiyo. Hata hivyo, nguvu za utawala wa jadi katika jamii ya Wairaqw zinaendelea kudhoofika kutokana na kuimarika kwa mifumo ya kisasa ya uendeshaji wa serikali hapa nchini.

Kisanaa, namna mojawapo ya kujieleza na kudokeza yale ambayo mtu huyafikiria katika jamii ya Wairaqw hujidhihirisha katika matumizi ya semi, hadithi na nyimbo (Norbustad, 1978). Pia, kuna ngoma ya ndani ambayo huchezwa wakati wa sherehe za harusi. Kwa mfano, wimbo wa Mudeli huimbwa wakati wa harusi. Ngoma nyingine ni ile ya nje ya mwaka huchezwa wakati wa mavuno. Ngoma hiyo huchezwa usiku kama ishara ya furaha na shukurani kwa Mwenyezi Mungu (Ramadhani, 2007). Mwaka unapoisha, Wairaqw wana utaratibu wa kufanya maombi ambayo huitwa ‘Slufay’ na ‘Giriyda’. Giriyda ni wimbo maalumu wa kuomba mambo mazuri na kuwaepusha kwa mabaya. Makala haya, hata hivyo, yamechunguza nafasi ya misemo ya jamii ya Wairaqw nchini Tanzania.

2.0 Nadharia, Mbinu na Upeo wa Makala

Uteuzi wa mada iliyopo katika makala haya umezingatia ukweli kwamba fasihi simulizi, ikiwemo misemo, inatazamwa kama wenzo thabiti wenyetunu na amali zinazorejelea kaida za kijadi zilizomo katika jamii mbalimbali. Data za msingi zilipatikana katika mkoa wa Manyara, Wilaya ya Mbulu Vijijini katika kata za Maghang (Magha Juu na Gidmadoy) na Labay (Basodarer na Labay). Maeneo hayo yameteuliwa kwa kuwa yana mawanda ya kutosha kupata data zilizolengwa ili kukidhi mahitaji ya

lengo kuu la makala. Mjadala wa data uliongozwa na nadharia ya Usosholojia. Nadharia ya Usosholojia iliasisiwa na Hippolyte Taine katikati ya karne ya 19 barani Ulaya (Wamitila, 2002). Mojawapo ya misingi yake ni kuichukulia fasihi kuwa ni kitengo pekee kilicho na uwezo wa kuakisi sayansi na utamaduni wa jamii unaodhibitiwa na miundo ya kijamii. Nadharia inaichunguza jamii kuwa ni malighafi ya fasihi; na kwamba, fasihi ina athari kubwa katika jamii inayohusika. Wasemaji wa misemo teule waliwekwa katika muktadha wao uliowazi ili kujua mwenendo na shughuli zao kwa kuwa misemo yao ni kiungo chao. Jamii ya Wairaqw iliwekwa katika ulimwengu wake wa kawaida na halisi ili kufanya uchambuzi wa kina. Pia, nadharia imetumika kuchunguza uhusiano uliopo baina ya fasihi na jamii kwa kurejelea misemo ya jamii teule.

3.0 Misemo katika Jamii ya Wairaqw nchini Tanzania

Misemo ni tungo za fasihi simulizi ambazo ni fupi fupi zenyе kutumia picha, tamathali na ishara. Misemo ni dhana ambayo hutumiwa kuelezea tungo, ambazo hutumia picha, ishara na tamathali ili kubeba maudhui yenye maana zinazofuatana na ibara mbalimbali za matumizi ya lugha (Nassoro, 2016). Pia, misemo hulinganisha maisha na matukio au vitu, pamoja na kutambulisha mazingira maalumu kupitia kazi ya fasihi inayohusika. Misemo imekuwa ikifanya kazi ya kusawiri maisha na kushughulikia masuala yanayomhusu binadamu pamoja na namna anavyoingiliana na mazingira yake (Mohamed, 2004). Misemo hutazamwa kama hazina ya urithi iliyosheheni hekima na maarifa ya jamii inayohusika. Maarifa yanayopatikana ni mionganoni mwa mambo ya msingi yanayojengwa jamii ili kumudu harakati za kimaisha.

Misemo hutazamwa kama matendo ya msingi ya binadamu. Muunganiko wa jamii na misemo yake huweza kuthibitishwa kihistoria na kiwakati. Hapana shaka kuwa kila utamaduni unaofahamika katika jamii mbalimbali za dunia una misemo yake inayoweza kubainishwa, kuchunguzwa na kuthibitishwa (Kyabashanga, 2018; Mbijima, 2011). Hali hiyo hutokana na kuwepo kwa muunganiko mkubwa kati ya misemo na maisha halisi ya kila siku ya mwanadamu wa sasa na wa tangu hapo kale. Misemo hutawaliwa na kuchukuliwa kama nyenzo ya kupambana na harakati za maisha ya kila siku katika jamii inayohusika. Misemo ina mengi yaliyo bora kulingana na jadi ya jamii inayohusika. Fasihi hutazamwa kama chombo cha kijamii kinachodhibitiwa na mahitaji ya jamii kiwakati. Jamii ya Wairaqw imechunguzwa kikamilifu jinsi ilivyofungamana na fasihi yake kama inavyodhahirika katika misemo yake.

3.1 Nafasi ya Dhamira katika Misemo ya Jamii ya Wairaqw

Dhamira ni ile jumla ya maana anayoivumbua mwandishi aandikapo; pamoja na maana anayoitambua msomaji au msikilizaji. Dhamira ni sehemu ya maudhui inayotuelekeza katika shabaha inayobainika tangu mwanzo hadi mwisho wa kazi ya kifasihi. Pia, dhamira ni mojawapo ya vipengele vinavyojenga utungo na kuunda maudhui katika kazi ya kifasihi. Maudhui katika kazi ya kifasihi hujumuisha vipengele vya dhamira, falsafa, migogoro, mtazamo, msimamo, na ujumbe (Mgogo, 2012). Katika makala haya tumechunguza kipengele cha dhamira zinazojitokeza katika misemo ya jamii ya Wairaqw. Makala yamewasilisha dhamira mbalimbali zilizomo katika misemo ya jamii teule kama zinavyojadiliwa katika sehemu zinazofuata.

3.1.1 Uaminifu na uadilifu

Dhamira mojawapo iliyopatikana katika misemo ya jamii ya Wairaqw inahusu umuhimu wa uaminifu. Uchunguzi wa dhamira hiyo ulizingatia mawanda mapana ya nadharia ya Usosholojia inayoitazama fasihi kama usawiri mkamilifu wa amali zilizomo katika jamii. Misemo katika jamii ya Wairaqw inasisitiza umuhimu wa uaminifu na uadilifu katika jamii. Msemo huu '*Tsir-ir-dayouso ka nii' yari*'(Ndege mwoga ana watoto wengi) unaifunza jamii kuепuka mambo yanayoweza kuyagharimu maisha. Ndege mwoga anachukuliwa kuwa anaweza kuwa na watoto wengi kutokana na uwoga wake. Jamii ya Wairaqw inachukulia kuwa mtu mwoga si mwepesi kutenda kinyume na kaida zilizopo katika jamii. Kwa kawaida, mtu mwaminifu mara nyingi hutekeleza jambo lililokubaliwa na jamii kwa kufuata mipaka ya makubaliano (Rajabu, 2012). Msemo huo huonesha wazi umuhimu wa uaminifu katika jamii kama nyenzo ya kuishi kwa amani na utulivu.

Pia, msemo mwingine unasema '*Mara kwaslemuser yari naqwariye*' (Nyumba za wapenda kesi wengi zinapotea) unatoa dhamira kuwa jamii na watu waliozoea kesi muda wowote maisha yao yanaweza kuharibika. Hali hiyo inatokana na kutokuwa na uaminifu na kuingilia mambo yasiyowahusu hali inayoondoa uaminifu katika jamii. Msemo huu hutoa taswira kuwa uaminifu ni jambo muhimu katika jamii. Mtu aliyezoea kuhalalisha ubatili na kuwa halali mwisho wake maisha yake huharibika pamoja na familia kukosa mwelekeo. Jamii haina budi kutenda haki ili kuепusha laana, lawama, chuki, visasi, na mafarakano yasiyokuwa ya lazima. Pia, msemo '*Slaa iakhmis*' (Kichaka kinasikia) unalenga kuishauri jamii kujenga uaminifu ili kuепuka migogoro isiyo na tija katika jamii. Jamii inapaswa kusema ukweli ili kumweka kila mmoja huru katika jamii. Msemo huu unasisitiza kuwa hakuna siri ya watu wengi.

Kumsema, hasa kumsengenya mtu kunaweza kusababisha kutolewana katika jamii (Kisanji, 2012). Uaminifu huwafanya watu kuishi huru na kutokuwa na wasiwasi katika jamii.

Vilevile, msemo unaosema ‘*Anu lach murue a buut*’ (Mimi ni mkali vitu vyangu ni vya kulipa), unasisitiza kuwa dawa ya deni ni kulipa. Hii inadhihirisha kwamba jamii ya Wairaqw inasisitiza haki na usawa na watu huishi kwa maadili waliyorithishwa kutoka vizazi tangu kale. Jamii hiyo inakataza kudhulumu amana isiyo ya halali. Jambo hilo linadhihirika mpaka miaka ya leo. Katika jamii hiyo, kwa mfano, mifugo hulala nje bila ulinzi wowote katika zizi lililozungushwa miiba na milango kuwekwa mti hali inayoakisi usalama, uaminifu na amani katika jamii. Msemo huu unaakisi hali halisi iliyopo katika jamii ya Wairaqw. Mtu akikopa amana ya mwingine katika jamii ni sharti alipe kabla hajachukuliwa hatua kwa mujibu wa jamii hiyo.

3.1.2 Hali ya uwajibikaji

Suala la umuhimu wa uwajibikaji katika jamii ya Wairaqw limeelezwa. Mjadala wa dhamira hiyo ulijikita katika misingi ya nadharia ya Usosholojia inayoitambua nafasi pana inayochukuliwa na muktadha wa kijamii katika uhakiki wa kazi za fasihi kwa kuzingatia umithilishaji wa hali zilizomo katika jamii. Msemo unaosema ‘*Qaymo bara nii yaa'b inos kos gi yaa'b*’ (Ukiwatuma watoto shambani, nao watawatuma watoto wenzao) una maana kuwa ukiwatuma watu wakafanye kazi bila kusimamiwa huzembea na kuharibika kinachofanyika. Kwa mfano, endapo wazazi na walezi watawaachia watoto waende kupalilia mazao shambani peke yao bila kusimamiwa, mazao yanaweza kuharibika. Wazazi wanapaswa kuwajibika na kusimamia shughuli yoyote inayofanyika ili kuepuka jambo lisiharibike. Watumishi wanalazimika kufanya kazi kwa bidii ili

uzalishaji uweze kuwa mzuri (Iheka, 2015). Wazazi wana jukumu la kuwafundisha kazi watoto wao na kuhakikisha kile walichowafundisha wamefanya vizuri kwa kuwafuatilia na kuwarekebisha kimaadili.

Katika msemo unaosema ‘*Matle a tlaghandi*’ (Asubuhi ni kiraka) unamaanisha kuwa shughuli yejote ya msingi ni vizuri ifanyike asubuhi ili kuifanya kwa ufanisi. Hali hii inatokana na ukweli kwamba mchana kuna hali ya kuchoka kutokana na juu kali. Kwa mfano, katika shughuli za kilimo, wakulima huanza kulima asubuhi na jioni huenda kumalizia sehemu iliyobakia. Aidha, ni vizuri kuwajibika asubuhi ili kuendelea kumudu changamoto mbalimbali zinazoweza kutokea baada ya asubuhi. Msemo huu unafanana na ule unaosema, ‘Asubuhi kazi, jioni mahesabu’ ukimaanisha kuwa asubuhi mtu huwa ana nguvu za kutosha baada ya kupumzika usiku; na muda wake ni mfupi mno ndio maana wakafananisha na kiraka. Ukiwajibika asubuhi, jioni utabaki kufanya tathmini kwa kile kilichofanyika mapema.

Pia, msemo huu ‘*Delor buhare a tsar*’ (Muda wa masika ni mbili) una maana kuwa muda wa masika ni mfupi, ukichelewa kulima na kupanda mapema hautapata mavuno ya kutosha kwa wakati. Kushindwa kumudu mahitaji ya wakati, watoto watapata njaa ili hali waliowahi kulima watapata mazao ya kutosha. Jamii inashauriwa kuzingatia muda na kulima kwa kufuata kanuni za kilimo na ufugaji ili kuhakikisha wanafanya kazi zao kwa kufuata misimu husika. Pia, jamii inapaswa kuwajibika ipasavyo kulingana na wakati ili kuepuka hali ya umaskini inayozandamana jamii nyingi hapa nchini (Buell, 2005). Kila jambo lifanyike mapema ili kumudu mahitaji ya jamii kwa wakati sahihi. Pia, msemo unaosema ‘*Sarhha tsuf a gaslay, qatso tsuf a gaslayka*’ (Uso unaotoa jasho hupata lakini

miguu iliyokaa haipati chochote' unasisitiza umuhimu wa uwajibikaji katika jamii. Kukaa bila kujihangaisha hakuwezi kumpatia mtu chochote. Jamii inapaswa kufanya kazi kwa kuzingatia hali halisi ya mazingira yao ya kiuchumi na kijiografia (Bwanamaya, 2004). Jamii isijiingize katika shughuli ambazo hazikubaliki katika jamii.

Msemo mwingine unaosema '*Ilwar sleer ghasarmo ki iwitananang'w wa wahahanka*' (Maziwa ya ng'ombe wa kuazima hayanyewi kwa kukaa) unasisitiza kuwa cha kuazima hakina manufaa ya kudumu. Jamii haina budi kufanya kazi kwa bidii ili kujenga uwezo wa kumiliki mali na vitu ambavyo ni zao lake. Kitu cha kuazima kitachukuliwa muda wowote pindi mwenye nacho atakapokihitaji bila kujali kama bado kinahitajika kwa aliyekiazima. Jamii ya Wairaqw hupendelea msemo huu wakimaanisha ukiazima ng'ombe au chochote kwa mtu yejote katika jamii hautakiwi kujisahau – ni sawa na *nguo ya kuazima haisitiri matako*. Wananchi lazima wafanye kazi kwa bidii na kuwajibika ipasavyo ili kuepuka kupewa misaada inayosababisha uvunjaji wa mila zetu na tamaduni zetu. Uvivu ni utumwa unaoondoa uwezo wa kujimini (Senyamanza, 2015). Rais wa awamu ya tano wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, hayati Dakt. John Pombe Magufuli, aliwahimiza wananchi wake wafanye kazi kwa bidii na maarifa ili kuepuka kutegemea misaada yenyenye masharti magumu kutoka katika mataifa ya nje yaliyoendelea kiuchumi na kiteknolojia.

3.1.3 Misingi ya uongozi na utawala

Dhamira nyingine iliyopatikana katika misemo ya jamii ya Wairaqw inahusu umuhimu wa uongozi bora. Mkusanyiko wowote wa watu ni lazima uwe na uongozi ili kuhakikisha mambo na mipango ya pamoja inakwenda vizuri. Kila jamii

inapaswa kuwa na uongozi imara utakaowasaidia kusukuma mbele gurudumu la maendeleo (Hassan, 2004; Mnyagatwa, 2009). Fasihi ni chombo kinachoihakiki jamii kikamilifu. Misemo hutumiwa kama chombo cha kuifunza, kuisahihisha na kuizindua jamii ili ifuate misingi inayotakiwa kuendelezwa na kuimarishwa katika harakati za maisha yake ya kila siku. Msemo unaosema '*Buhhtar wawtamo ador o'rotlor dirangw*' (Hasira za mtawala ni kama ngurumo ya simba) unasisitiza kuwa kiongozi anayechaguliwa kuongoza wenzake anaweza kufanya jambo lolote kulingana na mamlaka aliyonayo. Licha ya kuwa anapaswa kuwa na msimamo usioyumbishwa na yoyote katika kusimamia masuala mbalimbali ya kijamii. Pia, lazima kiongozi huyo atende haki kwa vitendo kwani anachokisema kisikilizwe na kufanyiwa kazi. Msemo huu unasisitiza namna ya kuwaheshimu viongozi, hasa katika mambo yote yenye tija katika jamii.

3.1.4 Umuhimu wa malezi

Dhamira nyingine iliyopatikana katika misemo ya jamii ya Wairaqw inahusu umuhimu wa malezi. Jamii yoyote ile ni lazima matendo yake yaende sambamba na utamaduni wake, mila na desturi zake, tabia na silka za jamii hiyo. Kwa mfano, msemo huu: '*Bawu bara si ari a sia*' (Ukikataa kuonywa kitakachokukuta utakataa) unamaanisha kuwa watu wanapaswa kukubali ushauri wanaopewa na watu wazima waliopo katika jamii yao. Msemo huu ni sawa na methali inayosema, 'Mkataa pema pabaya panamwita'. Wanajamii wanakumbushwa kufuata mambo yenye tija kwa manufaa ya familia na jamii zao. Pia, kuna msemo mwingine '*Baba o xwayla bir kahh o haraaye ikahi?*' (Baba wa kukuzaa kama hayupo, hata wa malezi hayupo?). Msemo huu unatoa picha kuwa malezi ya mtoto hayategemei kuwepo kwa wazazi wawili. Jamii nzima ina

jukumu la kuhakikisha watoto wanalelewa na kujengwa katika misingi ya uzalendo, utamaduni na maadili ya jamii (Hassan, 2010; Smart, 2007). Msemo huo unatoa taswira kuwa jamii ya Wairaqw inashirikiana kuwalea watoto kwa mujibu wa utamaduni wao. Mtoto ni mali ya jamii nzima. Msemo huu '*Puru khoslaro ahhoer faa' a 'tlemis iloa tsuu'*' (Unga uliosagwa ni rahisi kusonga ugali) unamaanisha kuwa jamii inapaswa kuwapa vijana malezi bora ili waweze kujitegemea katika jamii.

3.1.5 Upendo na amani

Upendo ni mionganini mwa mambo muhimu sana katika jamii yoyote ulimwenguni. Upendo huleta amani na kuchochea maendeleo katika ngazi ya familia, jamii na taifa (Kisanji, 2010). Mionganini mwa misemo iliyobeba dhamira hiyo ni pamoja na: '*Mangu tsui ti alen*' (Mguu wa mbu utupelee) unaomaanisha kuwa binadamu wanapaswa kupendana na kusaidiana katika hali ya raha na tabu. Kwa mfano, jirani akitembelewa anakula hata kama ni kidogo. Msemo huo una maana kuwa licha ya kuwa kilichopo ni kidogo, lazima wagawane kama sehemu ya kusaidiana. Msemo mwingine unasema, '*Yama imi ahembeto*' (Maeneo ya watu yabebwe kwa pamoja) humaanisha kuwa watu wasiharibu vitu vyatatu na wala mtu asisemwe ubaya kwani yote hayo huharibu upendo na kusababisha hali ya uvunjifu wa amani katika jamii. Jambo la msingi ni kuwafahamu watu na tabia zao ili kuweza kuishi kwa upendo bila kufarakana. Pia, katika msemo usemao, '*Hhae ial-a'ne, ial lagwalie*' (Ndugu wapendane wawe pamoja na wazae pamoja) msisitizo ni suala la upendo ili kujenga umoja na mshikamano katika jamii. Jamii ya Wairaqw inasisitiza ndugu na jamii nzima kupendana na kushirikiana ili kuondoa hali ya kuhitilafiana isiyo na tija kwa ustawi na uendelevu wa jamii.

3.1.6 Umuhimu wa kuweka akiba

Jamii yoyote ile inatakiwa ielimishwe kuhusiana na umuhimu wa kuweka akiba. Kuweka akiba huisaidia jamii kuwa na kitu kitakachowasaidia pindi linapotokea jambo la dharura, hasa njaa, magonjwa na maafa. Jamii ya Wairaqw inapenda kuweka akiba kwa kuhifadhi chakula chao katika maghala yanayotengenezwa nje ya nyumba. Wafugaji nao huhifadhi mafuta ya samli kwa kuwa wanajua kuwa malisho ya mifugo yao yatapungua kipindi cha kiangazi. Mfano wa msemo unaoakisi hali hiyo ni: '*Bara amoker ghumta lohi huek*' (Ukienda sehemu beba kibuyu cha njiani) unaosisitiza umuhimu wa kujiwekea akiba ili kuepuka fedheha kwa kuwa matatizo hayapigi hodi. Binadamu yejote anatakiwa kujiandaa katika maisha yake kwani safari ni hatua moja baada ya nyingine. Maisha ni safari iliyojaa adha kadha wa kadha, ambazo henziepukiki. Jamii haina budi kuweka akiba itakayomsaidia mtu anaposafiri ili waliobaki nyumbani waendelee kuishi vizuri. Jamii inapaswa kufanya kazi kwa bidii ili kuweka akiba itakayosaidia kumudu harakati za maisha ya kila siku katika jamii.

3.1.7 Hekima na busara

Dhamira nyingine iliyopatikana katika misemo ya jamii ya Wairaqw inahusu umuhimu wa busara. Hekima na busara katika jamii humfanya binadamu aweze kukabiliana vyema na mazingira yanayomzunguka. Msemo unaohusiana na hekima na busara katika jamii ya Wairaqw hunasema, '*Do a sleer yae tlakw a tsegamis*' (Nyumba ni sawa na ng'ombe mwenye mguu mbovu) ukimaanisha umuhimu wa kuwa na subira katika jamii. Wazazi wanapaswa kuishi kwa subira kwani wanandoa wanapokutana na kuishi pamoja kila mmoja na tabia zake zinazoweza kusababisha kuhitilafiana. Uamuzi wa busara

unatakiwa kabla ya kulifanyia kazi jambo lolote (Senzighe, 2004). Pia, msemo huu: ‘*Kuro tsihay u gawta tsahh*’ (Mwewe mwenye mimba utamtambua juu) unasisitiza kuwa baadhi ya maneno hayatamkwi hadharani bali hutumia lugha ya uficho ili kulinda staha za jamii inayohusika. Hali hiyo huisaidia jamii kutenda haki na kutumia busara katika kusuluuhisha masuala fulani fulani katika jamii. Jamii hiyo hutumia wazee na wanajamii kwa jumla ili kufanya suluhu katika jamii kwa busara ya hali ya juu bila ubaguzi wa aina yoyote.

Pia, msemo unaosema, ‘*Do bura qwareska dir masombimar uqwares dir seemir a'wak*’ (Usipopoteza nyuma ukiwa kijana utapoteza ukizeeka) unasisitiza kuwa kijana anaweza kupambana ili kuyabadili maisha yake mabaya kwa kufanya kazi kwa juhudhi na maarifa kabla ya kuzeeka. Uzee humfanya binadamu yejote kupoteza mambo mengi, hasa nguvu, maarifa na kumbukumbu (Wambua, 2011). Jamii inatakiwa kusisitiza malezi ya familia yanayozingatia miiko na maadili ya jamii. Pia, msemo unaosema kuwa ‘*Gaw masomba gwareesi gwa ehat*’ (Uwindaji wa vijana, tai huwafuata) humaanisha kuwa vijana wana uwezo wa kufanya jambo lolote zuri au baya. Busara za wazazi huwapa fursa pana ya kufuatilia kile walichokiona kibaya na kuomba msamaha kwa yejote aliyetendewa. Jamii ya Wairaqw inaamini kuwa kutenda haki kunaepusha laana, visasi na mafarakano. Katika msemo huo, wazee wanafananishwa na tai kwa kuwa anaheshimiwa sana katika jamii hiyo. Wazazi hawana budi kuwaongoza vijana kwa ustawi na uendelevu wa jamii na kizazi chao.

3.1.8 Subira na uvumilivu

Dhamira inayohusu umuhimu wa subira pia inajitokeza katika misemo ya jamii ya Wairaqw. Kwa kawaida, jamii inapaswa kuishi katika misingi ya uvumilivu. Mtu kukosa uvumilivu

katika jamii si jambo jema kwani anaweza kuangukia katika hali ambayo haikukusudiwa. Jamii ya Wairaqw ina misemo inayotumika kuielimisha jamii ili iweze kuwa na subira, hasa namna ya kuyashughulikia mambo katika hali ya kutokuwa na papara kama inavyoelezwa katika msemo usemao, ‘*Nanagi doos gu ghoer*’ (Mdudu wa mahindi atafika tu kwake). Mdudu huyo hutembea polepole, lakini atafika tu anakokwenda. Jambo lolote hata kama lina ugumu kupita kiasi, ipo siku litafanikiwa, hasa kama litawekewa misingi imara inayoonesha namna bora ya kulitekeleza kwa nadharia na vitendo (Darco, 2006). Kwa hakika, ‘Mwenda pole hajikwai’, na ‘Mvumilivu hula mbivu’.

4.0 Hitimisho na Mapendelekezo

Makala yamechunguza kipengele cha dhamira zilizomo katika misemo ya jamii ya Wairaqw nchini Tanzania. Baadhi yake zinahusu masuala ya uaminifu, uwajibikaji, uongozi, dharaui, busara, upendo, akiba, na subira katika jamii. Dhamira zilizomo katika misemo ya jamii hiyo ni mojawapo ya chombo imara cha kijamii kinachoihakiki jamii katika misingi ya kuielimisha na kuuelewa muktadha mpana wa jamii iliyochunguzwa. Kwa muhtasari, dhamira hizo zinatazamwa kama maktaba mahsusii ya urejelezi wa masuala ya kijamii; na kiungo thabiti cha kiasili kinachojenga mfumo wa kuifunza, kuiimarisha na kuiweka jamii pamoja katika misingi ya utamaduni na falsafa nzima ya maisha tangu kale mpaka sasa.

Marejeleo

- Buell, L. (2005). *The future of environmental criticism: Environmental criticism and literary imagination.* Malden: Blackwell Publishing.
- Bwanamaya, B. J. (2004). *Uhusiano kati ya methali na mabadiliko katika jamii.* Dar es Salaam: Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.
- Darko K. A. (2006). *Ecocriticism and environmental knowledge of Asante oral traditional poetry.* PhD Dissertation, University of Witwatersrand.
- Hassan, N. (2010). *Mitindo ya matumizi ya lugha: Utafiti katika semi za bajaji.* Tasnifu ya Shahada ya Umahiri. Dar es Salaam: Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.
- Hoja, K. (2004). *Misemo na methali na vita dhidi ya UKIMWI katika jamii ya wasukuma.* Tasnifu ya Shahada ya Kwanza. Dar es Salaam: Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.
- Iheka, C. (2015). *African literature and the environment: A study in postcolonial ecocriticism.* Phd Thesis, Michigan State University.
- Kamera, W. D. (1988). *Firro na slufay: The traditional litanies of the Iraqw.* African Study Monographs.
- Kisanji, J. (2012). *Kufuwawa kwa miiko na kupotoka kwa maadili: Uchunguzi kifani wa jamii ya Wabungu.* Tasnifu ya Umahiri. Dar es Salaam: Chuo Kikuu Huria cha Tanzania.
- Kisanji, J. A. (2010). *Miiko ya jamii ya Wabungu.* Dar es Salaam: AKADEMIYA /AERA Kiswahili Researched Products.

- Kyabalishanga, F. (2018). *Dhima ya methali za Wahaya*. Shahada ya kwanza. Dar es Salaam: Chuo Kikuu Huria cha Tanzania.
- Mbijima, R. J. (2011). *Dhima ya visasili katika kabila la Wagogo*. Shahada ya Umahiri. Dar es Salaam: Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.
- Mgogo, Y. P. (2017). *Kuchunguza hadithi za Wanyiha katika kurithisha elimu ya jadi*. Shahada ya Uzamivu. Dar es Salaam: Chuo Kikuu Huria cha Tanzania.
- Mnyagatwa, T. K. (2009). *Tungizi za Mnyagatwa*. Dar es Salaam: Al Amin Educational and Research Academy (Akademiya).
- Nassoro, H. (2016). *Semi katika vyombo vya safari vya bahari Kisiwani Pemba*. Dar es Salaam: Chuo Kikuu Huria cha Tanzania.
- Norbustad, F. (2002). *Historia fupi ya Wairaqw*. Aldin Inverstment (T) Limited.
- Nordbustad, F. (1978). *Nchi ya Wairaqw ilivyoanza*. Mbulu Tanzania: Christian Literature Centre.
- Polit. D. (1999). *Creativity and change among the Iraqw of Northen Tanzania*. Thesis, Master of Arts in Social Anthropology. University of Bergen.
- Rajabu, A. (2012). *Misemo ya Kiswahili katika vazi la fulana: Uchambuzi wa dhamira na matumizi ya lugha*. Shahada ya Umahiri. Dar es Salaam: Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.
- Ramadhani, M. H. (2007). Mapokeo ya Wa-Iraqw Mbulu. Unpublished Manuscript.

- Sengo, T. S. (2008). *Tafakuri ya utu na uhai*. Dar es Salaam: Huda Publishers.
- Senyamanza, C. A. (2015). *Tathmini ya mabadiliko ya rara mintarafu maendeleo ya jamii: Uchunguzi katika Mkoa wa Songwe*. Shahada ya Uzamivu. Dar es Salaam: Chuo Kikuu Huria cha Tanzania.
- Senzighe, R. (2004). *Usawiri wa mwanamke katika methali za Wapare*: Tasinifu ya Umahiri. Dar es Salaam: Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.
- Smart, C. (2007). *Personal life*. Cambridge: Polity Press.
- Thornton, J. R. (1980). *Space, time and culture among Iraqw of Tanzania*. London, UK: Academic Press.
- Wambua, M. S. (2001). *Mtindo wa nyimbo za Kakai Kilonzo*. Tasinifu ya Shahada ya Umahiri. Kenyatta University.
- Wamitila, K. W. (2002). *Uhakiki wa fasihi, misingi na vipengele vyake*. Nairobi: Phoenix Publishers.